JUNIOR SCHOOL ASSESSMENT TEST

PIONEER MARK SERIES

GREDI YA NANE - 2025

KISWAHILI

Jina: _____

Shule: _____ Nambari ya usajili. _____ Tarehe: _____

VIWANGO VYA KUZINGATIA KATIKA KUTATHIMINI.

KUZIDI MATARAJIO	KUFIKIA MATARAJIO	KUKARIBIA MATARAJIO	MBALI NA MATARAJIO	JUMLA (ALAMA %)
35-50	26-34	15-25	0-14	

SEHEMU YA A: UFAHAMU

Soma Makala yafuatayo kisha ujibu maswali

Ni jambo lisiliopingika kuwa elimu ni ufunguo wa maisha. Aidha elimu ni nguze imara ya kuegemea maishani hata hivyo, yafaa ifahamike kuwa elimu itamfaidi mmiliki wayo yule ambaye ataitumia kwa ufasaha. La muhimu zaidi yule ambaye ataitumia kwa nidhamu, hekima na heshima

Haijalishi iwapo mahuluki ameyasoma matopa ya vitabu. Haijalishi amefika kiwango kipi au anazo shahada zipi? Iwapo hana adabu, heshima, nidhamu na uajibikaji elimu yako haijakamilika. Elimu hiyo yote si lolote si chochote. Elimu yake itakuwa kama pambo wala si lebasi. Pambo haliwezi kusitiri mtu. Hiyo ni kazi ya nguo.

Ni fedheha na izara kuwaona baadhi ya insi wakichachawiza kuwa wameelimika ilhali wanazo fuska. Heshima kwao ni mwiko. Adabu kwao ni neno geni. Ukweli ni kuwa elimu hiyo yao haina faida kwa walimwengu. Mwalimu wangu wa zamani alinieleza kuwa kumiliki elimu ya aina hiyo ni sawa na kufunga tai huku mtu akiwa uchi wa mnyama.

Ni jambo aula mtu kuonyesha elimu yake kwa vitendo. Vitendo vya yeyote aliye na elimu vinafaa view na mwelekeo na vya kutamanika. Vionyeshe ustaarabu wala si ushenzi.

Aidha ifahamike kuwa elimu si ya vitabu tu. La hasha! Ipo pia elimu dunia. Sharti elimu yetu ituwezeshe kutafakari ya dunia

MASWALI

1. Ni jambo lipi lisilopingika kuhusu elimu (al 1)

   .....

2. Ni nani anayefaidika sana na elimu aliyo nayo(al 1) .....
3. Elimu bora ni ipi?
   A) Ya chuo kikuu B) Yenye uajibikaji C) Ya nyumbani D. Inayoheshimiwa
4. Mtu hutajika ameelimika ikiwa (al 1)
   A) Amesoma matopa ya vitabu
   B) Ana msururu wa shahada
   C) Ana fuska
   D) Ana ustaarabu
5. Ni kweli kusema (al 1)
   A) Yeyote aliye na elimu ni mstaarabu
   B) Asiye na elimu ni mshenzi
   C) Matendo mema hupita elimu
   D) Elimu si ufunguo wa maisha